



TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA
Kitalu Na. 339, Mtaa wa Nyerere - Kilimani
S.L.P 1049, DODOMA/ 285, ZANZIBAR
Simu: +255 734 047 775/734 119 978; (24) 2230494 (ZNZ)
Barua Pepe: info@chragg.go.tz; zanzibar@chragg.go.tz
Tovuti: www.chragg.go.tz

Desemba 9, 2021

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Tamko la THBUB wakati wa kampeni ya siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto, 2021

TANGU Novemba 25 mwaka huu nchi mbalimbali duniani, ikiwemo Tanzania zimekuwa katika Kampeni ya Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia Dhidi ya Wanawake na Watoto. Lengo kuu la kampeni hizi zitakazohitimishwa Desemba 10, 2021, siku ambayo ni kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Haki za Binadamu Duniani, ni kuongeza uelewa wa jamii ili kukomesha vitendo vya ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto.

Kampeni hizi zilianza kufanyika kwa mara ya kwanza mwaka 1991 kufuatia maandamano ya wanaharakati yaliyoongozwa na taasisi ya kimataifa ya wanawake viongozi nchini Marekani. Hadi sasa mashirika zaidi ya 6,000 kutoka nchi 187 duniani yamekuwa yakishiriki katika kampeni hizi.

Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) inaungana na wadau mbalimbali kote duniani katika kampeni hizi zilizobeba kauli mbiu isemayo: **“Ewe Mwananchi komesha ukatili wa kijinsia sasa.”** Lengo la kauli mbiu hii ni kumkumbusha kila mtu katika jamii kuhusu wajibu alionao wa kuhakikisha kuwa vitendo vya ukatili nchini vinapungua au kumalizika kabisa.

THBUB inatambua hatua mbalimbali zilizochukuliwa na zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika kuhakikisha kuwa wanawake na watoto wanalindwa dhidi ya vitendo vyote vya ukatili wa kijinsia. Hatua hizi ni pamoja na kuweka mifumo thabiti ya kisera, kisheria na kiutawala.

Pamoja na jitihada hizo, zipo changamoto kadhaa zinazokwamisha juhudi za Serikali katika kukabiliana na ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto nchini katika jamii na kupelekea ongezeko la ukatili huo katika maeneo ya kaya, biashara, masoko na vyuo. Changamoto hizi ni pamoja na kuendelea kuwepo kwa vitendo vya ukatili, mila potofu, kuwepo kwa sheria ambazo zinaupungufu katika kulinda haki za wanawake na watoto, na uelewa mdogo wa jamii.

Kufuatia hali hiyo, THBUB inapendekeza yafuatayo:

- i) Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali waendeleo kutoa elimu kwa jamii ili kuongeza ulinzi kwa wanawake na watoto dhidi ya vitendo viovu vinavyofanywa dhidi yao;
- ii) Wizara ya Katiba na Sheria iendeleo kufanyia maboresho Sheria mbalimbali, ikiwemo Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 ili kukuza na kulinda haki za wanawake na watoto; na
- iii) Wananchi watekeleze wajibu wao wa kuheshimu na kulinda haki za wanawake na watoto hapa nchini.

THBUB inaaahidi kushirikiana na wadau wote katika kuhakikisha kuwa haki za wanawake na watoto zinafahamika, zinaheshimiwa na kulindwa.

“Ewe Mwananchi komesha ukatili wa kijinsia sasa.”

Imetolewa na:



Dkt. Fatma Rashid Khalfan

Kamishna

TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA

Desemba 9, 2021